

## Informasjon om situasjonen rundt Koronavirus i Fjellregionen.

### Habari kuhusu hali ya virusi vya Korona hapa Fjellregionen.

Kama inavyojulikana ugonjwa wa Korona umeshafika hapa kwetu wilayani. Kwa bahati mbaya tuna upungufu wa vyombo vya vipimo, na hatuwezi kuwapima watu wote wenye dalili ya ugonjwa huu. Watu wengi wanaweza kuwa na virusi vya korona bila ya kujitambua, na pia hatuwezi kufuatilia ugonjwa ulipoanzia.

Kwa sababu hizo, ni muhimu sana ukijisikia kuumwa, ukae ndani, na upunguze kadri ya uwezo wako kukutana na watu unaoishi nao. Ni lazima ukae nyumbani na uepukane kukutana na watu wengine mpaka upone. Watu wanao ishi na wewe wanaweza kutoka nje kama hawana dalili za ugonjwa au wameshauriana na daktari.

Kama ukiona umezidiwa, na unahisi unahitaji kuongea na daktari, unaweza kuwasiliana na daktari wako wa pekee. Piga simu

Ukipatwa na virusi vya Korona na unahitaji msaada, utafuatiliwa na daktari na nesi kwenye simu.

Serikali imetengeneza sheria, watu gani watakao pimwa virusi vya Korona. Watu pekee watakao pimwa ni wenye dalili ya maambukizi ya mapafu.

Watu watakao pimwa ni:

- 1) Wale wanao umwa sana na kuhitaji kulazwa hospitali
- 2) Wale wanao ishi kwenye taasisi za afya
- 3) Wale wanaofanya kazi na wagonjwa au wazee
- 4) Wale Zaidi ya miaka 65 wa kikundi cha hatari
- 5) Watu walio kutana na mgonjwa wa virusi vya Korona ambayo imethibitishwa

Wagonjwa pekee ndio watakao pimwa, kwa sababu virusi vya korona vinachukuwa mda kuonekana.

Dalili ya ugonjwa wa korona ni homa, kukohowa, kuumwa na mwili, matatizo ya kuhema na kuumwa na koo.

Ni muhimu kufuata ujumbe unaotoka serikalini.

Nawashukuru sana

Tor Halvor Bjørnstad-Tuveng

Swahili

Daktari mkuu wa wilaya ya Tynset